Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MBILI

**Kikao cha Thelathini na Nne – Tarehe 29 Julai, 2008**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi*)

## D U A

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

## T A N Z I A

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mara nyingine tena katika uhai wa Bunge letu hili umeniangukia wajibu wa kuwatangazieni habari ya masikitiko kwamba mwenzetu Mheshimiwa Chacha Zakayo Wangwe, amefariki jana usiku saa mbili na dakika hamsini na tano.

Amefariki kwa ajali ya gari katika barabara ya kutoka Dodoma kwenda Dar es Salaam baada ya gari yake aina ya *Toyota Corolla* aliyokuwa akiiendesha kupinduka pale Pandambili ikaacha njia, ikabingirika mara kadhaa na imekata miti yaani imegonga miti na kwa hiyo aliumia sana na akafa pale pale.

Mheshimiwa Chacha Wangwe alikuwa na abiria mmoja rafiki yake anayeitwa Bwana Deus Malya, yeye amesalimika na yupo hapa Dodoma na Ofisi imeweza kuongea naye.

Hatuna maelezo ya ziada kwa niaba yenu nasimama kuwapa pole familia ya karibu ya Mheshimiwa Chacha Zakayo Wangwe, wananchi wa Tarime na hususani wapiga kura, Chama chake yaani Mwenyekiti na chama cha CHADEMA na wote ambao tunaguswa kwa karibu na kifo hiki.

Kwa mujibu wa Kanuni ya 149 inasema hivi; “Endapo Mbunge atafariki wakati Bunge likiwa katika shughuli zake, Spika ataahirisha shughuli za Bunge kwa siku hiyo kwa ajili ya maombolezo.”

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, kwa kuzingatia Kanuni hiyo sasa naliahirisha Bunge hadi saa sita kamili mchana. Tume tupokee taarifa ya jinsi ya kumsindikiza mwenzetu. Ahsanteni sana!

Ningesema kwa kweli nimesitisha tu kwa sababu tunakutana tena saa sita mchana. Naomba sasa Kamati ya Uongozi na Tume ya Huduma za Bunge tukutane Ukumbi wa Spika mara baada ya hapa.

*(Saa 03.03 asubuhi Bunge lilifungwa mpaka saa 6.00 mchana)*

*(Saa 06.00 mchana Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Kamati ya Uongozi na Tume ya Huduma za Bunge tumekutana kikao cha pamoja na dharura tumekuwa wakati wote tukiwasiliana na familia ya Marehemu na maamuzi tuliyokubaliana kwa pamoja ni kama ifuatavyo:

Kwanza, ni kwamba mazishi yatakuwa keshokutwa yaani siku ya Alhamisi tarehe 31 Julai, 2008 adhuhuri kijijini Kyamakorere, kilometa 12 Kutoka Tarime.

Leo hii Ofisi ya Bunge imekodi ndege itakayowaleta wafiwa kutoka Dar es Salaam kuja hapa, bahati nzuri Mjane wa Marehemu amekwishafika aliondoka alfajiri kule Dar es Salaam. Mheshimiwa Profesa Wangwe na ndugu wengine wamekwishapita Morogoro wanakuja huku Dodoma. Kwa hiyo, uwakilishi wa wanafamilia utakuwa umekamilika kufikia majira ya saa nane mchana, watoto wawili kama nilivyosema wapo hapa hapa Dodoma.

Kwa hiyo, utaratibu wetu kuanzia jioni leo utakuwa kama ifuatavyo;

Tunawaomba Waheshimiwa Wabunge Saa 9:30 alasiri leo tuje mbele ya Jengo hili jipya la Bunge kwenye ngazi na mtakuta sasa maturubai na viti vya kutosha na mpangilio wa namna ya kuketi pale. Sasa saa 10:00 jioni mwili wa Marehemu utawasili kwenye viwanja vya Bunge. Saa 10:15 tunamtazamia Rais wa Jamhuri ya Muungano, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete atawasili kwenye eneo la Bunge.

Mwili utawekwa kwenye ile nafasi ya wazi baada tu ya kumaliza ngazi na utakuwa kama kawaida yaani sanduku litakuwa na Bendera ya Taifa.

Salamu zitatolewa kama ifuatavyo; kwanza ni salamu fupi kutoka Kambi ya Upinzani, baada ya hapo Mheshimiwa Waziri Mkuu atatoa salamu za Serikali na nitamalizia kwa maneno mafupi kwa niaba yenu. Wakati tunadhani itakuwa takriban saa 10.35 au 10.40 jioni, tutaanza kutoa heshima za mwisho.

Kabla ya kutoa heshima za mwisho mwili utaingizwa katika eneo lile nje ya mlango huu mkuu wa kuingia yaani eneo lile ambalo huwa tunasalimiana yaani baada ya chombo cha usalama. Tutaingilia mlango mmoja na kutokea mlango mwingine kwa mzunguko kama ilivyo kawaida katika kutoa heshima za mwisho. Mpangilio utaelezwa ni dhahiri kwamba kutakuwa na itifaki kwa kuanzia Mheshimiwa Rais na wengine tutafuata, *Inspector General* wa Polisi anakuja na *helicopter*, Jaji Mfawidhi wa Dodoma na Majaji wa Dodoma watakuwepo na wengine tutakaowaona ambao wamependa kuja kushiriki nasi na pengine watapata nafasi ya kwenda Tarime.

Tunadhani shughuli hiyo itakwisha mnamo saa 12.00 jioni na mwili utaondolewa kurejeshwa hospitali kwa ajili ya kuhifadhiwa ili kesho kwa ndege maalum saa 01.30 asubuhi Waheshimiwa Wabunge wawili pamoja na wanafamilia tunakadiria 18 wataondoka na mwili kuelekea Musoma, nimeongea na Mkuu wa Mkoa ili pale Musoma magari yawepo kuweza kufikisha msafara mzima Tarime.

Tumeteua kwa uwakilishi Waheshimiwa Wabunge 20 wao wataondoka siku ya mazishi saa 1.30 asubuhi orodha tutawaarifu na sasa hivi nadhani wamekwishaarifiwa. Wabunge wote wa Mkoa wa Mara, Wabunge watatu wa Kambi ya Upinzani lakini akiwepo pia Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Kiongozi wa sisi Wabunge kwa bahati mbaya mimi binafsi nitashindwa kwa sababu nalazimika keshokutwa kwenda Malaysia kwa sababu ya uchaguzi kwa sababu mimi pia ni mgombea.

Naibu Spika, analazimika kwenda Njombe kwa sababu kuna ziara ya Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati ya Madini ambayo Marehemu Mheshimiwa Chacha Zakayo Wangwe alikuwa Mjumbe, Mheshimiwa William Shellukindo yeye akiwa Mwenyekiti wa Kamati lakini pia kama mnavyofahamu ni Kamishna wa Tume atakuwa ndiye mwakilishi wetu kiongozi kwenye mazishi hayo.

Kwa hiyo, ukiacha yeye sasa tumechagua kwa mujibu wa jinsia na uwakilishi humu kutoka Bara na Visiwani ndiyo wanatimia Wabunge 20. Ni dhahiri watakuwepo na watumishi wa Bunge ambao watashiriki saa 01.30 asubuhi siku ya Alhamisi tarehe 31 Julai, 2008 kusafiri kwa ndege hiyo maalum hadi Musoma na wao sawia kupokelewa na uongozi wa Mkoa wa Mara kwa ajili ya mazishi saa za adhuhuri na baadaye watarejea kwa ndege hiyo hiyo kurudi Dodoma ili kuendelea na shughuli nyingine.

Kwa hiyo, ni dhahiri kwamba kesho asubuhi tutaendelea na shughuli ambazo imebidi ziahirishwe kwa kumuita Mtoa Hoja, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ili aweze kuwasilisha hotuba yake baada ya kipindi cha Maswali na Majibu.

Zaidi ya hivyo, ningependa tu kusema kwamba katika kushughulikia mwili wa Marehemu tahadhari zimechukuliwa kwa sababu ni ajali lazima uchunguzi wa kitaalamu ufanyike, hii ndiyo kawaida kwa vifo vya aina hii. Kwa hiyo, ndiyo maana mnaona mambo yanaelekea kwenye saa kumi kwa sababu sasa hivi yule *Chief Pathologist* kutoka Muhimbili anakaribia kuwasili. Atashirikiana na Daktari Mkuu wa Dodoma, mwanandugu mmoja, Afisa wa Bunge mmoja na Polisi ndiyo kawaida ili washuhudie uchunguzi wa mwili ndiyo maana tunakawia.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, baada ya taarifa hiyo sasa naliahirisha Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 06:09 mchana Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatano Tarehe 30 Julai, 2008 saa tatu asubuhi)*